**Title: Under the Mango Trees**

**EPISODE 9**

**Author: Romie Singh**

**Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun**

**List of characters for episode 9:**

- Narrator
- Desirée
- Eric
- Alice
- Lorraine
- Sazi
- Grandma
- Endurance
- Bongo

Karibu kwenye sehemu ya tisa ya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Mchezo wa redio kwa jina Chini Ya Miembe. Tunaangazia maswala yanayohusu njia za kupanga uzazi na Uzazi Kwa Mpango. Hususa kuhusu vijana na jinsi watakavyo jikinga na mimba zisizo takikana, virusi vya HIV na magonjwa ya zinaa kwa kutumia njia mbali mbali za kinga.Sababu kubwa ya pingamizi dhidi ya njia za kuzuia ujauzito ni ukosefu wa ufahamu, kutokujali afya na jamii kutotambua njia hizo. Katika bara la Afrika kuna idadi kubwa ya vifo vya kina mama waja wazito,Idadi kubwa ya uzazi inayohatarisha maisha ya vijana na ukosefu wa usawa wa jinsia ambao unasababisha wasichana wadogo kutiwa

mimba. Makala hizi zina lengo la kufafanua maswala haya nyeti kwa matumaini ya kuanzisha mjadala. Leo hii Desirée anaendeleza juhudi zake za kumtafuta baba yake na anakaribia kumpata.

SIG.TUNE UP HOLD UNDER AND FADE

**1. NARRATOR:** Lorraine alikuwa anajiuguza maumivu yake ya siri. Kwa siku kadhaa sasa amekuwa anahofia kujiuliza iwapo kweli ni mja mzito au La? Alitakikana asiwe na wasiwasi wowote kwa sababu alikuwa anatumia tembe. Lakini anafahamu fika kuwa alisahau kumeza tembe zake hizo zaidi ya mara moja. Sasa ameshajua ukweli kuwa ana mimba. – Matokeo ya kifaa cha kupima mimba alichokinunua yameonyesha kuwa yeye ni mja mzito.

**<u>Scene 2 In the bedroom</u>**

| | |
|---|---|
| **1.** SAZI: | Lorraine, mimi bado nakupenda. Ninatamani kama nisinge kuwachia wewe peke yako kufuatilia maswala ya kinga ya uja uzito. Hata mimi nilipaswa kutumia Kondom. |
| **2.** LORRAINE: (sobbing) | Oh, Sazi – samahani sana mpenzi. Sikutaka haya yatokee. Ninafikiria juu ya mashindano ya Pop Idols . Ninataka sana kushiriki lakini Bongo akijua kuwa mimi ni mja mzito, bila shaka atanitoa. Alinieleza hilo wazi pale mwanzoni. |

**3.** SAZI: Achana na Bongo! Sisi tuangalie yanayotuhusu kwa sasa, Lorraine. Tutafanya nini? Yaani mimi hata sina wazo lolote kwa sasa nimechanganyikiwa. Sijui sisi sote kwa pamoja tuzungumze na mama yako au vipi?

**4.** 4. LORRAINE: Mama yangu? Ndio, nadhani yeye ataweza kutuelewa zaidi kuliko mtu mwingine yeyote. Hebu wacha tumuite aje hapa chumbani kwangu. nisingetaka Eric anione jinsi nilivyo.

**5.** **SFX:** MUSIC UP. FADE IN DIALOGUE:

**6.** LORRAINE: Jamani hata sijui nitafanya nini kuhusu diploma yangu shuuleni? Nikiamua kubaki na uja uzito basi lazima nitafukuzwa shule. Mama yangu! Sijui niitoe? (sobbing heavily)

**7.** SAZI: Shhh, usilie mpenzi. Tuliza moyo wako.

**8.** ALICE: Mwanangu mpenzi, kumbuka kwamba wewe na Sazi mnapendana. Una familia yake na sisi familia yako pia tuko pamoja nawe. Yaani pande zote ziko pamoja nawe kwa hali na mali.

**9.** SAZI: Mimi nakuhakikishia kuwa nitakuwa baba mwema, najua mama yangu pia atanisaidia. Tutafaulu tu mpenzi.

**10.** ALICE: Kumbuka wewe ni kijana bado una miaka 18 tu, kwa hivyo unayo nafasi ya kufanya diploma yako baadae. Mimi mwenyewe nitakusaidia pia. **(kissing Lorraine)** Usibabaike huu sio mwisho wa dunia......!

**11.** MUSIC UP

**NARRATOR:** Maisha ya Lorraine yanachukua mueleko mpya jata ya Desirée ingawa kwa mulekeo tafauti. Desirée alikuwa anajitahidi kufanikisha mipango ya kumtafuta baba yake. Endurance alikuwa na hamu kubwa ya kumpata baba yao, haya nyanya nae alifurahia juhudi za Desirée.

**<u>Scene 3.</u>**

**12.** GRANMA: Baba yenu aliahidi kuwa atafungua biashara mpya halafu atakuja kuwachukua. Endurance, zidisha subira, mpe muda.

**13.** ENDURANCE: Lakini sasa tunajua anakofanyia kazi. Desirée ameshaipata namba yake ya simu. Mimi nataka kumuona baba tena.

Nyanya nataka kumsaidia baba katika gereji yake, sitaki kuendelea kuchunga ng'ombe hapa shambani.

**14.** DESIRÉ: (laughing) Woa! Pole pole! Hatua kwa hatua! Eric anayo namba yake ya simu. Subiri mpaka atakapo kuja.

**15.** ENDURANCE: Eric anakuja? lini?

**16.** DESIRÉ: Atakuja wakati wowote kutokea sasa. Hebu chungulia nje uone kama anakuja.

**17.** **SFX:** Endurance runs off in excitement.

**18.** ENDURANCE: (off mic) tutamuona tena baba yetu ! Tutamuona tena baba yetu!

**19.** GRANMA: Endurance anafuraha sana sasa, nafikiri hata shuleni pia. Wewe ni dada mzuri na mama pia! Oh, vipi maendeleo ya ile karatasi ya maswali niliyotia saini? Ile ambayo mlipewa na mwalimu wenu mkuu wiki chache zilizopita? Si wazazi walitakana wajaze kwa ajili ya kuwasaidia walimu wafahamu kuhusu hali ya wanafunzi katika familia zao, walisema eti itawaimarisha wanafunzi kwenye masomo yao.

**20.** DESIRÉ: Mkurugenzi wa shule bwana Adams, ataitisha mkutano wa shule hivi karibuni. Hapo utapata nafasi ya kukutana na walimu wetu pamoja na wazazi wengine.

**21.** GRANMA: Vizuri. Ninahitaji kuzungumza na walimu na vijana. Lakini pia kusikiliza, maanake! Ai! Vijana wa siku hizi wanabadilika kwa haraka.

**22.** **SFX:** cell phone ring

**23.** DESIRÉE: Oh! Sijui ni Eric huyo anapiga ? Hallo? ...Naam?..... Bongo?

**24.** BONGO: (telephone voice) Sasa? Husikii sudi inakuita, Desirée?

**25.** 4. DESIRÉE: Sudi? Una maana gani?

**26.** 5. BONGO: Ok. Umekaa? Hebu vuta pumzi!

**NARRATOR:** Alichokieleza Bongo kwa Desirée kweli kilitwaa pumzi zake. Lorraine ametoka kwenye mashindanot! Lakini kwa nini. Au kwa sababu gani? Bongo hakujua kabisa . Lorraine alisema tu kuwa ilikuwa ni kwa sababu za kimazingira, “ambayo yalizidi upeo wake” Na hapo gari ikawasili.

| | | |
|---|---|---|
| **27.** | **SFX:** Car horn | |
| **28.** | ENDURANCE: (off mic) Des – Eric ameshafika! | |
| **29.** | DESIRÉE: (As if waking from a dream) Eric? Eric! | |
| **30.** | **SFX:** Running /breathless | |
| **31.** | ERIC: | Des! Kuna nini? |
| **32.** | DESIRÉ: | Bongo anasema lazima nishiriki kwenye mashindano ya – Pop Idols! |
| **33.** | ERIC: | Wow! Hiyo ni habari nzuri! |
| **34.** | DESIRÉE: | Lorraine amejitoa lakini Bongo anasema hajui ni kwa sabbau gani! Je wewe unajua? |
| **35.** | ERIC: | Eti Lorraine amejitoa? Hapana, hata sina habari. Mbona hiyo ni habari mpya. |
| **36.** | DESIRÉE: | Lakini Eric, mimi siwezi kushiriki kwenye mashindano hayo ya Pop Idols labda mpaka tumpate baba yangu na mjomba Blessing. Bongo ameniambia lazima niamue katika saa 24. |

| | | |
|---|---|---|
| **37.** | ERIC: | Hii ni fursa ya ajabu, Des. Huwezi kukosa safari hii. Hebu chukua! Mpigie baba yako sasa hivi. Usijali kuhusu muda wa mazungumzo. Mpigie! |
| **38.** | DESIRÉE: | Natumai kuwa hii namba ni sahihi, Oh. Jamani! akikataa je? |
| **39.** | **SFX** Dialling tone: | |
| **40.** | DESIRÉE: | Hallo – Huyo ni baba? |
| **41.** | ENDURANCE: | Baba? Hebu wacha niseme nae! |
| **42.** | DESIRÉE: (softly) | Endurance, ngoja kidogo. (louder) Baba? Endurance na mimi tumesubiri mawasiliano kutoka kwako..........Oh!.......Lakini una mahala pa kuishi sasa?.......Oh....Hapana, sisi tuwazima. Sikiliza, Baba, Ni habari ndefu, lakini nataka nikuulize jambo la muhimu. |
| **43.** | ERIC: (Whispering) | Muulize kama Endurance anaweza kubaki kwake jumamosi ijayo. Na pia muulize mjomba Blessing yuko wapi. |
| **44.** | DESIRÉE: | Baba? (NOISE) Oh, mawasiliano yanakatika katika! |

**NARRATOR:** Eric na Endurance walijawa na shauku wakati Desirée alipojaribu kumpigia tena baba yake aliye katika katika mji wa Granville. Wakati huo huo katika mjini Kentown, Bongo alijawa na wasiwasi mwingi pia, wakati akisubiri majibu kutoka kwa Desirée, iwapo atashiriki kwenye mashindano ya Pop Idols au La. Hakufahamu bado kile Lorraine alichomwambia kuwa ni "mazingira yaliyo zidi upeo wake" lakini sasa ameshampigia Desirée na kumwomba ashiriki. Je akikataa tena? Na itakuwa vipi ikiwa mazingira hayo ya Lorraine yatarudi kuwa sawa nae awe anataka kuendelea kushiriki kwenye mashindano? Bongo atayajua yote hivi punde!

**Scene 4 In the office.**

**45.** **SFX:** Background pop music playing; fax machine; office phone ringing; cell phone ring tone. Phone FX on Lorraine's voice throughout

**46.** BONGO: Rainbow Agency. Bongo anazungumza. Hallo.

**47.** LORRAINE: (Phone FX) Bongo, Ni mimi.

**48.** BONGO: Lorraine, baby. Hey! Nafurahi kusikia sauti yako tena! Vipi?

**49.** LORRAINE: Bongo, Nakuomba, samahani sana, najua kuwa ulinitegemea mimi. Yaani najisikia vibaya sana kuwa nimekukosea.

| | | |
|---|---|---|
| **50.** | BONGO: | Sikiliza, mpenzi. Hebu niambie tu kuwa utashiriki na mimi nitafurahi sana. |
| **51.** | LORRAINE: | Kwani hujamwambia Desirée ashiriki badala yangu? |
| **52.** | BONGO: | Yeah, nimemwambia lakini si unajua kuwa hakufiki kwa lolote – na siajabu akakataa. Wee unawajua tu hawa wasichana wa kijijini, wanapenda sana kubaki nyumbani wakati wote. |
| **53.** | LORRAINE: | Nasikitika, Bongo, sina sifa tena za kushiriki. Nili… unajua… Nilikuwa nameza tembe za kuzuia ujauzito lakini … hivyo hivyo nimeshika mimba. |
| **54.** | BONGO: | Aiaiai. Una mimba! Lorraine. Hapo hakuna njia nyingine yaani moja kwa moja wewe hufai kushiriki. Nilikuonya lakini, tangu mwanzo! Nilikwambia tumia kinga. Kitu gani kilitokea? Ulikosa kumeza tembe siku moja au vipi? |
| **55.** | LORRAINE: | Kitu kama hicho. Angalia, Bongo, familia yangu pamoja na ya Sazi zimenihakikishia kuwa zitanisaidia. Kwa hivyo mimi nimeamua kuilea mimba yangu hadi nitakapo pata mtoto pia nimlee. Pengine |

mpaka baada ya miaka miwili au mitatu ndio nitakuwa na muda, je nikija kukugongea utanifu….

**56.** BONGO: Bila shaka! Ikiwa kweli unaamini kuwa unataka kuwa mwimbaji/mwanamuziki basi endelea na mazoezi nyumbani, Nakuhakikishia tutafanya mpango tu utakapo kuwa tayari. Usisahau pia nyimbo ni nzuri sana kwa watoto. Zinawaburudisha na zinawatuliza. Muimbie tu mtoto nyimbo taaamu na wala hatakusumbua hutapata shida kupata mwangalizi wa mtoto yaya!

**NARRATOR:** Bongo alifahamu wazi sasa kuwa, Desirée lazima achukue nafasi ya Lorraine! Aliisikiliza tena sauti yake aliyoinasa kwenye studio yake. Alikuwa mshindi! Lakini je atakubali kushiriki? Aliongeza sauti ya muziki. Atahitaji muda gani kufanya uamuzi? Jibu lilihitajika haraka.

SIG TUNE UP (Desire singing)

**OUTRO.**

Na mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa mchezo wa leo katika NOa Bongo Jenga Maisha Yako, " Chini Ya MIembe" ni mchezo wa redio uliotungwa na Romie Singh. Jiunge nasi katika sehemu ya kumi nay a mwisho wakati ambapo Desirée anatambua kuwa kuitimiza ndoto yake ya kuwa mwanamuziki kunategemea kwanza ampate baba yake.

Kumbuka unaweza kuusikiliza tena mchezo huu, Au pia mwambie rafiki yako ausikilize. Anuani yetu ya mtandao ni :d w world dot de mkwaju l b e

Hadi wakati ujao, baki salama.

**END OF EPISODE NINE**